**Noa Bongo ! Jenga Maisha Yako !**

**Utandawazi : Wasanii na Mtandao**

**Autor : (O-Töne + Text) :Yann Durand**
**Redaktion : Sandrine Blanchard**
**Übersetzun : Anne Thomas**

---

**Wi immer 2 Stimmen - Sauti 3**

- **junger Sprecher 1 …………..Msimulizi wa kiume 1**
- **junge Sprecherin 1 …………Msimulizi wa kike 1**
- **Sprecher(in) 2…………. …….Msimulizi wa kike 2**
- **als Off –Stimme für die Reportage**

---

**Für die O-Töne dazu :**
**1 junge Frau (Satz)**
**1 junger Mann (5 Otöne)**
**1 Mann (2 Otöne )**

---

**Vorspann LbE………………………Kiashirio cha Kipindi**

**SEHEMU YA KWANZA – REPORTAGE : REPOTI**

**Msimulizi wa kike 1 :** Habari gani !

**Msimulizi wa kiume 1 :** Natumai nyote hamjambo ! Leo katika mafululizo wa vipindi vyetu juu ya utandawazi tutazungumzia muziki.

**Msimulizi wa kike 1 :** Na tutakuwa tunaelekea katika mji wa Düsseldorf nchini Ujerumani.

**Msimulizi wa kiume 1 :** …….ambapo tutakutana na msanii kutoka Guinea.

**LBE SBY 1…………………………..**

Kipaji kina faida lakini kipaji hakiwezi kununuliwa.

**Msimulizi wa kike 2 :** Düsseldorf ni mji mkubwa ulioko kwenye kingo za Mto Rhine. Flingem ni wilaya mashuhuri ilioko mashariki mwa mji huo ambapo miaka mitatu iliopita shirika moja liliasisiwa kuwasaidia vijana.Maabara ya kompyuta ya Teknolojia ya Habari IT na mkahawa wa mtandao yameleta mabadiliko makubwa tokea wakati huo hivi ndivyo anavyofafanuwa Thomas Thönes mtu mwenye umbo la maguvu mwenye chapa ya tatoo mwilini mwake na mwenye kuvaa herini.Akiwa na umri wa miaka ya thelathini taswira yake hiyo inavuta heshima.Yeye ni muasisi na rais wa shirika hilo.

**LBE SBY 3 (Deutsh ………Kijerumani )…………..**

Watoto na vijana wanaweza kuchezesha CD za majaribio bure wanaweza kuchukuwa masomo ya kuimba,kujifunza namna ya kutumia ala za muziki na pia tunaka kuanzisha mafunzo ya kucheza muziki.Tunaka kuwaunga mkono vijana katika fani hizo zote ……..teknolojia ya sauti,muziki,kuimba na kadhalika.

**Atmo : LBE SBY 4 Freestyle ………………..**

Leo SBY pamoja na wanamuziki wengine vijana ni sehemu isiokosekana ya kampuni ya kurekodi muziki ya TM Records…Rekodi ya Juu Ya Muziki …chapa ambayo imetengenezwa mjini Düsseldorf ambao ni mji ulioko mbali na nchi alikozaliwa kijana huyo SBY.Alivumbuwa shauku yake mjini Conakry kabla ya hata kutimiza umri wa 17.

**LBE SBY 5**

Kulikuwa na onyesho kubwa sana la Daara J na Killpoint. Nilkuwa kijana sana na nilikuwa na furaha kweli kuliona kundi hilo na hapo nikaanza kufikiria …..kwamba unajuwa ni lazima ufanye kitu. Siku za awali za SBY na kundi lake la kwanza Cible du ghetto lenye kutafsiriwa kama Ghetto Target zilikuwa ngumu.Ilibidi awashawishi

wazazi wake ambao hawakufurahia wazo kwamba mtoto wao wa kiume atakuja kuwa mwanamuziki wa mtindo wa rapu.SBY na marafiki zake walijitengenezea jina katika maonyesho ya muziki ya Kiafrika lakini ilikuwa ni vigumu kufanikiwa nchini Guinea.

**LBE SBY 6**

Kwa serikali muziki wa rapu ulikuwa ni mchafu sana.Walidiriki hata kusema kwamba sisi ni kundi la wahuni la wahalifu.Sio rahisi kwa vijana wa Guinea kujielezea wenyewe kwa sababu kile kinachotolewa na radio na televisheni huchujwa.

**Msimulizi wa kike 2 :** Mazingira hayo yamefanya iwe vigumu kuruka kuingia katika sayari ya muziki wa mtindo wa hip hop:Baada ya kusomea juu ya uchumi kwa mwaka mmoja aliondoka kwenda Ulaya.Alikuwa karibu kabisa kujaaliwa kubakia Ufaransa ambapo alikuwa na familia.Lakini hatimae aliichaguwa Ujerumani ambapo baba yake mhandisi alikuwa akifanya kazi.Juu ya hivyo mama yake ambaye ni mkemia anafanya kazi na Wajerumani nchini Guinea.

**Atmo : LBE SBY 7 Freestyle …………….**

**Msimulizi wa kike 2 :** Muziki ulitimiza dhima kubwa katika maisha ya SBY.Hujisikia kufarajika kuwemo katika jamii kubwa ya muziki huo wa mtindo wa hip hop na hususan akiwa na familia yake ya kampuni ya TM Records ambayo sambamba na kampuni ya Westside ya Ujerumani hivi karibuni zilitanuka na kuingia kwenye soko la mtandao jambo ambalo limemfurahisha Thomas Thönnes.

**LBE SBY 8 (Deutsch……….Kijerumani)**

Kampuni ya Westside Germany imefuata upepo na kutaka kujihusisha zaidi katika kuwasaidia vijana hususan katika fani ya kuwaendeleza wasanii kwenye jukwaa la mtandao.Huwasaidia kuanzisha kurasa zao mtandaoni kwa mfano kwenye tovuti ya Myspace au kuanzisha tovuti zao wenyewe.

**Msimulizi wa kike 2 :** Myspace ni tovuti ya kimataifa ya kushirikiana kanda za video. SBY kabla ya hapo alikuwa haijuwi tovuti hiyo wakati huo akiwa bado yuko nchini Guinea.Lakini rafiki yake mmoja huko Düsseldorf alimjulisha kwa haraka juu ya tovuti hiyo.

**LBE SBY 9**

Nilimwambia niache nifanye maonyesho yangu ….na kwamba Myspace ni kwa ajili ya watoto.Na alisema hapana Myspace ni muhimu sana.Kwa hiyo nilisema sawa nitaangalia.Na halafu ikabidi nianzishe ukurasa wangu mwenyewe wa mtandao ……ambao ulikuwa ukiitwa Myspace .com SBY kwa ajili ya Lakhara………Na baadae nikafanya maonyesho ya muziki wa jukwaani mjini Düsseldorf,Duisburg,Cologne,Dortmund na hata Berlin.Hapo ndipo nilipofikiria kwamba iwapo unafanya maonyesho ya muziki kwa nini usiyaingize kwenye filamu?

**Msimulizi wa kike 2 :** Kujenga taswira ni muhinu kwa wasanii.Leo hii ujumbe ambao muimbaji anautuma unakuwa unahusiana sana na muziki wake na maudhui kadhalika taswira yake pamoja na kuwepo kwa vyombo vya habari.Mtandao unaweza kumsaidia SBY Mjerumani wa asili ya Guinea ambaye anarapu kwa Kifaransa na Kingereza na kujitangazia jina duniani kote.

**LBE SBY**

Watu wamekuwa wakiniandikia kutoka kila mahala kutoka Ufaransa,Ujerumani,Ubelgiji,Marekani.Naishukuru tovuti ya Myspace na Your Tube ama kweli dunia hii ni adhimu.Dunia ni kitu kilichokamilika! Hauna haja tena ya kuwasiliana na watu ambao wanaogopa ushindani au wanaohodhi mfumo mzima, ulimwengu mzima wa shughuli za muziki.Ukiwa na Myspace unakuwa huru na unaweza kujitangaza mwenyewe.Ni kutokana na Myspace watu nchini Marekani wamependekeza kwamba nitengeneze sauti za muziki pamoja nao.

**Msimulizi wa kike 2 :** Wasanii wote katika kampuni ya TM Records wana matumaini ya pamoja kwamba wataukwaa umashuhuri kwa

msaada wa mtandao.Jumi ni kijana wa kike kutoka Nigeria na pia Sierra Leone.Sio tu anataka kufanikiwa bali anataka kuwa muimbaji nyota.

**LBE SBY 11 (English ……….Kingereza )**

Kwa kweli kazi ninayoifanya ni adhimu na mbingu haitokuwa mwisho wa safari yangu.

**Musik : LBE SBY 12 french Contact (Ende des Stücks) ………………………..**

**MWISHO WA SEHEMU YA KWANZA**

---

**SEHEMU YA PILI      ERKLÄRSTÜCK**

**Msimulizi wa kiume 1 + Msimulizi wa kike 1 tu**

**Msimulizi wa kiume  :  ( sings …..anaimba )**

*(Baby you can drive my car) 'Yes, I'm gonna be a star'.      (kutoka wimbo wa kundi la the Beatles unaoitwa 'Drive My car')*

**Msimulizi wa kike :** Alaa …….unajuwa kwamba uko hewani!

**Msimulizi wa kiume :** Ohh samahani ! Sawa nitafanya mazoezi baadae …..kwa sababu nataka kuonyesha muziki wangu kwenye MyBase.

**Msimulizi wa kike :** MY SPACE !

**Msimulizi wa kiume :**  Ohoo ….lakini hasa hicho ni kitu gani ?

**- 7 -**

**Msimulizi wa kike :** Ni jukwaa katika mtandao.Unatakiwa tu kuwa mwanachama ili uweze kuwa na ukurasa wako mwenyewe binafsi wa

mtandao na kuwasiliana na dunia nzima.Wale wasiokuwa wanachama wanaweza kukaguwa kurasa za tovuti tafauti .

**Msimulizi wa kiume :** Kurasa ambazo wanachama wanaweza kuweka vitu vyao, nyimbo zao,video na kadhalika ?

**Msimulizi wa kike :** Ndio na kurasa hizo zinakuwa na mfumo wa kutuma ujumbe ambapo inamaanisha kwamba watumiaji wa mtandao wanaweza kubadilishana picha na maoni.Unaweza ukajua watu wangapi wametembelea tovuti yako.

**Msimulizi wa kiume:** Kwa hiyo MySpace ni mashuhuri duniani kote?

**Msimulizi wa kike :** Hasa hasa imeanzishwa nchini Marekani hapo mwaka 2003…….miaka miwili baadae tayari ilikuja kuwa mojawapo ya tovuti zinazotembelewa na watu wengi sana duniani.Hivi sasa ina watumiaji milioni 300 waliojiandikisha.

**Msimulizi wa kiume :** Lakini iwapo kila mtu huwa anaweza kuweka kila kitu kwenye mtandao lazima hapo patakuwa na vitu vingi ambavyo sio vizuri?

**Msimulizi wa kike :**

Jambo hilo ni kweli na mara nyingi wahakiki wamekuwa wakisema hivyo.Lakini kungelikuwa hakuna magunduzi mengi ingelikuwa mtandao hauko wazi kwa kila mtu.

**Msimulizi wa kiume :** Unataka kusema kwamba wanamuziki wa ridhaa ambao wamekuwa mashuhuri kwa ghafla kumetokana na mtandao?

**Msimulizi wa kike :** Hasa! Mtandao pia huvutia nadhari ya makampuni makubwa ya muziki yenye kutengeneza na kusambaza rekodi.Iwapo msanii anafanikiwa katika mtandao.

**Msimulizi wa kiume :** Yaani kampuni zinakuwa zinamkimbilia.Ni jambo zuri juu ya kwamba kwa sababu wasanii wasio wa kawaida hupata nafasi ya kujulikana.

**Msimulizi wa kike :**

Inaweza kusemwa kuwa sio jambo baya.

**Abspann ………………..Funga Kipindi……………**

Na kufikia hapo ndio tumefikia mwisho wa kipindi chetu cha Noa Bongo! Jenga Maisha Yako!Ahsante kwa kusikiliza kipindi hiki juu ya utandawazi na matumizi ya mtandao katika kuwaendeleza wasanii.Ni kipindi cha Deutsche Welle kilichotayarishwa na Yann Durand.Ili kujuwa zaidi au ukitaka kusikiliza tena kipindi hiki tafadhali nenda kwenye tovuti yetu www.dw-world.de/be
Usikose kujiunga nasi tena mara nyengine ! Kwaheri!
Kwaheri !